Kioo cha Lugha, Juz. 24(1), 22-39
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v24i1.2

Ruwaza za Sinonimu zenye Asili ya Kiarabu katika Kiswahili: Mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 4* (2019)

George Jerald Kitundu[1]

Ikisiri

Lugha ya Kiswahili ina muwasala wa muda mrefu na lugha mbalimbali za kigeni kama Kiarabu. Kuwapo kwa muwasala huo kumesababisha lugha ya Kiswahili kukopa maneno mengi kutoka lugha hiyo (Mbaabu, 2007; Gibbe, 2010). Maneno katika lugha hukopwa kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi ya sababu hizo ni kukosekana kwa msamiati unaosimamia dhana ngeni ambazo hazifahamiki katika lugha pokezi na kasumba ya wazungumzaji kukopa maneno kutoka lugha za kigeni hata kama msamiati unaokopwa ulikwisha kukopwa kutoka lugha hiyo ya kigeni (Kiango, 1999). Matokeo ya ukopaji huo husababisha lugha kuwa na maneno mawili au zaidi yanayohusiana kimaana kutoka lugha ngeni moja. Hali hii husababisha kuibuka kwa sinonimu. Lugha inapokuwa na sinonimu mbalimbali husababisha kuibuka kwa ruwaza za sinonimu. Makala hii inachunguza ruwaza za sinonimu zenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, *Toleo la 4* (KKS4) (2019). Ili kufikia azma ya kuchunguza ruwaza hizo, data za makala hii zimekusanywa kutoka kwenye kamusi tajwa. Ukusanyaji wa data umefanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Data zilizokusanywa zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya maudhui na kuongozwa na Nadharia ya Vijenzi Semantiki. Kwa ujumla, makala hii imebaini kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza sita za sinonimu za mkopo kutoka Kiarabu. Ruwaza hizo ni ruwaza ya uwili, ya utatu, ya unne, ya utano, ya usita na ya usaba. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu maneno ya mkopo yanavyoibua sinonimu kutoka lugha nyingine kama Kiingereza, Kihindi au Kiajemi ili kubaini ruwaza zake.

1.0 Utangulizi


Ukopaji wa maneno katika lugha ni suala linalochangia ongezeko la msamiati katika lugha pokezi. Msamiati hukopwa katika lugha kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kasumba ya watumiaji wa lugha kukopa maneno wanapotagusana na jamii ngeni (Kiango, 1999). Ukopaji wa namna hii husababi-


[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: george.jerald@yahoo.com

sha kuwapo kwa maneno mengi ya mkopo katika lugha pokezi hata kama kuna maneno ya asili au ya mkopo yenye dhana ileile ya neno linalokopwa. Lugha ya Kiswahili imekopa msamiati kutoka lugha mbalimbali za kigeni kama Kiarabu, Kiingereza, Kijerumani, Kihindi, Kiajemi na Kireno. Kati ya lugha hizo, Kiarabu kimechangia kwa kiasi kikubwa maneno mengi katika lugha ya Kiswahili. Haya yanaelezwa na baadhi ya wataalamu kama Bosha (1994) na Mbaabu (2007) kuwa Kiswahili kimeathiriwa na lugha mbalimbali kama vile Kihindi, Kiarabu, Kireno na Kijerumani lakini athari za Kiarabu zimezidi na zinaendelea hadi leo. Maelezo haya yanathibitisha kuwa kuna maneno mengi ya mkopo katika Kiswahili kutoka katika Kiarabu na bado kuna ongezeko la ukopaji wa maneno kutoka lugha hiyo kutokana na kuwapo kwa mwingiliano katika shughuli mbalimbali. Hali hii ya kukopa maneno kutoka lugha moja husababisha kuwe na maneno mawili au zaidi yanayorejelea dhana ileile. Maneno hayo ndiyo hufahamika kama sinonimu. Sinonimu kutoka lugha moja huhusisha seti mbalimbali kama za uwili au utatu kulingana na idadi ya maneno yaliyokopwa (Kitundu, 2022). Hali hii ya kuwapo kwa maneno mawili, matatu au zaidi yenye maana sawa huibua ruwaza za sinonimu ambazo zinatokana na idadi ya maneno katika seti ya sinonimu. Makala hii inachunguza ruwaza za sinonimu zenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 4* (KKS4) (2019). Ili kufikia azma hiyo, makala hii imegawanywa katika sehemu sita. Sehemu ya kwanza inatoa utangulizi wa jumla kuhusu makala. Sehemu ya pili inafafanua dhana ya sinonimu na namna ukopaji wa maneno unavyoibua sinonimu. Sehemu ya tatu inabainisha mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Sehemu ya nne inabainisha nadharia iliyoongoza uchambuzi wa data. Sehemu ya tano inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za ruwaza zilizobainika, na sehemu ya sita inatoa hitimisho la makala hii.

2.0 Dhana ya Sinonimu

Watalaamu mbalimbali wamefasili sinonimu kuwa ni maneno mawili au zaidi yenye maana sawa au zinazokaribiana (Cruse, 2006; Danglli, 2010; Resani, 2015; Chacha na Malangwa, 2019; Kahigi, 2019). Chacha na Malangwa (2019) wanaeleza kuwa sinonimu ni maumbo mawili au zaidi yanayokaribiana sana katika maana ambayo pengine huwa na sifa ya kubadilishana hata nafasi katika sentensi. Sinonimu katika lugha hugawanywa katika makundi mawili; sinonimu kamili na sinonimu zisizo kamili (Ndimele, 1997; Resani, 2015; Kahigi, 2019; Chacha na Malangwa, 2019). Sinonimu kamili ni zile zinazofanana kimaana na kimatumizi wakati sinonimu sizizo kamili zinafanana katika baadhi ya dhana tu. Chacha na Malangwa wanatumia vielelezo vifuatavyo kutofautisha sinonimu kamili na zisizo kamili.





Kielelezo Na. 1: Sinonimu Kamili **Kielelezo Na. 2: Sinonimu Zisizo Kamili**

Chanzo: Chacha na Malangwa (2019) na Vimeboreshwa[2] na Mtafiti (2024)

Vielelezo Na. 1 na 2 vinaonesha aina mbili za sinonimu. Kwanza, kuna sinonimu kamili ambazo maneno husika huwa na sifa za kisemantiki zinazofanana. Maneno yenye sifa ya usinonimu kamili hubadilishana nafasi katika miktadha yote bila kuathiri maana. Katika Kielelezo Na. 1, maneno A na B yana sifa sawa ndiyo maana yamo ndani ya duara moja kuonesha kuwa maana na matumizi ni sawa. Kwa upande wa sinonimu zisizo kamili, maneno yake huchangia au hufanana katika baadhi ya dhana au virejelewa tu. Katika kielelezo Na. 2 maneno A na B yanafanana au kuingiliana kwenye baadhi ya dhana au sifa tu kama AB inavyoonekana. Makala hii inachunguza sinonimu za mkopo zinazohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu.

Sinonimu hutokana na sababu mbalimbali kama vile usanifishaji wa maneno ambapo kila taasisi husanifisha istilahi zake kama ilivyo kwa maneno *shule* (Tanzania Bara) na *skuli* (Zanzibar); na mitindo mbalimbali ya lugha kama vile ya kidini na kitaaluma. Sababu nyingine za kuibuka kwa sinonimu ni urejeleo wa kijinsia, tofauti za kilahaja, matumizi ya tasfida na ukopaji wa maneno (Matinde, 2012; Resani, 2015; Chacha na Malangwa, 2019). Kati ya sababu hizo za kuibuka kwa sinonimu, sababu inayofafanuliwa zaidi katika makala hii ni ukopaji wa maneno kwa kuwa ndicho chanzo kimojawapo cha kuwapo kwa sinonimu za mkopo katika lugha. Kipengele kinachofuata kinafafanua ukopaji wa maneno hususani, kutoka Kiarabu na namna ukopaji huo unavyoibua sinonimu.

2.1 Ukopaji wa Maneno ya Kiswahili kutoka Kiarabu

Ukopaji wa maneno ni uchukuaji wa maneno kutoka lugha nyingine kisha kuyaingiza na kuyatumia katika mfumo wake au katika lugha pokezi (Kiango, 1999). Karibu kila lugha hukopa maneno kutoka lugha mbalimbali pindi kunapokuwa na muwasala wa jamiilugha mbili au zaidi (Kiango, 1999; Hoffer, 2005; King'ei, 2010). Maneno katika lugha hukopwa kutoka lugha ambazo kiisimu ziko katika familia moja kama ilivyo kwa Kiswahili hukopa maneno kutoka lugha nyingine za Kibantu ambazo zina mnasaba nayo au kukopa kutoka lugha za kigeni ambazo zinatofautiana kiisimu kama ilivyo kwa Kiswahili kukopa

[2] Uboreshaji uliofanyika ni kuonesha mwingiliano wa dhana katika maneno mawili tofauti na kielelezo cha awali ambacho mwingiliano haukuwekwa bayana na neno moja ndilo lililoonekana kuingiza sifa zake katika neno lingine.

kutoka Kiarabu au Kiingereza.

Maneno hukopwa katika lugha kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni: mahitaji ya msamiati katika lugha kwa ajili ya kuelezea dhana fulani. Grey (1964), Kiango (1999) na Matinde (2012) wanafafanua kwamba ukopaji wa neno hufanyika ikiwa neno linalokopwa linasimamia dhana au kitu ambacho hakikuwa kinajulikana katika jamii ya lugha hiyo. Sababu ya pili ni kuwapo kwa mwingiliano wa nguvu za kisiasa ambazo husababisha jamii kutumia maneno ya lugha tawala, na hivyo, kuongeza msamiati katika lugha tawaliwa hata kama msamiati unaoelezea dhana hiyo ulikuwapo au ulikwisha kukopwa (Robins, 1964; Chuwa, 1988). Sababu ya tatu ni msamiati hukopwa kutokana na kasumba ya wazungumzaji wa lugha fulani kupenda kukopa msamiati kutoka lugha mbalimbali licha ya kuwapo kwa msamiati unaorejelea dhana zinazokopwa (Kiango, 1999; Matinde, 2012). Maelezo hayo yanaonesha kwamba ukopaji unaotokana na kasumba ya watu pamoja na kutawaliwa kwa nguvu na jamii zenye nguvu kisiasa, ndio unaosababisha kuibuka kwa sinonimu katika lugha pokezi.

Suala la ukopaji wa maneno ya Kiswahili kutoka lugha mbalimbali za kigeni, hususani Kiarabu limeelezwa na wataalamu wengi. Kati yao, wapo ambao wameelezea hali ya ukopaji kwa kutumia asilimia za maneno ya mkopo kutoka Kiarabu katika Kiswahili. Mathalani, Krumm (1940) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imekopa maneno mengi kutoka Kiarabu. Maneno hayo yanakadiriwa kuwa ni asilimia 30. Mohamed (2010) anaeleza kuwa lugha ya Kiarabu imechangia maneno kwa asilimia 19 inapoilinganishwa na maneno kutoka lugha zingine na yale ya asili. Makadirio ya wataalamu hawa yanaonesha kwamba Kiswahili kimekopa maneno mengi kutoka Kiarabu.

Chiraghdin na Mnyampara (1977) na Chuwa (1988) nao wanaeleza kuwa lugha ya Kiarabu ndiyo yenye maneno mengi katika Kiswahili kuliko lugha ya taifa lolote lingine la kigeni. Sababu kubwa ni kuwa bara Arabu ndiyo nchi ya kigeni iliyokuwa jirani zaidi na upwa wa Afrika Mashariki na watu wake waliingiliana sana na Wabantu kuliko watu wengine. Maelezo ya Chiraghdin na Mnyampara (1977) na Chuwa (1988) yanaonesha kuwa Waarabu ndio waliochangia maneno mengi katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa walikutana nao katika shughuli mbalimbali kama biashara na kuoana. Hivyo, kuna maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu katika lugha ya Kiswahili.

Bosha (1994) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imekopa maneno kutoka Kiarabu. Bosha anataja mifano kama vile *zaka, sadaka, itikadi,* na *imani*. Maelezo na mifano ya Bosha vinaonesha kuwa kulikuwa na maneno mawili au zaidi katika uwanja mmoja unaorejelea dhana ileile, yaani sinonimu. Hivyo, ni wazi kuwa ukopaji wa maneno kutoka Kiarabu umesababisha kuwe na maneno mawili au zaidi yenye maana sawa, yaani sinonimu, jambo ambalo linachunguzwa katika makala hii ili kubaini ruwaza za sinonimu zinazojitokeza katika maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu.

Shembilu (2017) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imekopa msamiati kutoka lugha mbalimbali za kigeni kama Kiarabu. Ukopaji huu unatokana na muwasala uliopo baina ya Waswahili na Waarabu. Waarabu walianza kufanya muwasala na Waswahili tangu karne ya mwanzoni kabisa (Mbaabu, 2007; Gibbe, 2010; na Habwe, Matei na Nyonje, 2010). Muwasala huo ulihusu biashara na dini. Shembilu (2017) anaendelea kueleza kuwa muwasala huo ulisababisha Kiswahili kisiepuke kuathiriwa na Kiarabu katika viwango mbalimbali. Athari kubwa inayojitokeza kutokana na mtagusano huo ni msamiati.

Mzamir (2021) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imekopa maneno mengi kutoka Kiarabu. Maneno hayo yameingizwa katika kamusi kupitia muwasala baina ya Waarabu na Waswahili karne nyingi zilizopita (Ahmad, 2021). Anaendelea kueleza kuwa katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili* Toleo la 2 (KKK2) kuna maneno 2,647 yenye asili ya Kiarabu. Idadi hii ni sawa na asilimia 10.76 ya vidahizo vyote 24,600 vilivyopo kwenye KKK2. Mzamir (2021) anatoa mifano kama *sadaka* na *dhabihu* (*kitu chochote kinachotolewa kwa Mungu au mizimu kwa ajili ya jambo fulani*); na *abadan* na *asilan!* (*hata kidogo*). Kati ya maneno hayo, yapo maneno mawili au zaidi kutoka Kiarabu ambayo yana maana sawa, yaani sinonimu.

Kwa ujumla, mapitio ya maandiko mbalimbali yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili imekopa maneno kutoka lugha ya Kiarabu. Kutokana na ukopaji huo kuna maneno mawili au zaidi yenye maana zinazofanana au kukaribiana, yaani sinonimu. Sinonimu katika lugha hazijakaa kiholela bali hufuata ruwaza fulani. Ruwaza hizo, hususani zinazohusisha maneno ya mkopo kutoka lugha moja kama Kiarabu, bado hazipo bayana kwa kuwa haifahamiki kuna ruwaza gani za sinonimu za mkopo kutoka Kiarabu. Kwa hiyo, kulikuwa na haja ya kuchunguza zaidi suala hili ili kubaini ruwaza zinazojitokeza. Dhana ya ruwaza za sinonimu inatumiwa katika utafiti huu kama mpangilio wa sinonimu kulingana na idadi ya maneno katika seti moja ya sinonimu. Kwa hiyo, kigezo kikuu kinachotumika katika kupanga maneno yenye sifa ya usinonimu ni idadi ya maneno yanayorejelea dhana au kitu kilekile. Hii ina maana kuwa kama kuna maneno mawili yenye kufanana kimaana yanawekwa kwenye ruwaza ya uwili na yakiwa matatu yanawekwa kwenye ruwaza ya utatu.

3.0 Medhodolojia ya Utafiti

Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 4* (2019). Uteuzi wa kamusi hii unatokana na kuwapo kwa taarifa za msingi zinazohitajika katika utafiti huu ambazo ni etimolojia ya vidahizo sambamba na sinonimu. Mbinu ya ukusanyaji wa data iliyotumika kukusanya data katika matini teule ni uchambuzi wa matini. Matini teule ilipitiwa kisha vidahizo vya Kiswahili vyenye asili ya lugha ya Kiarabu ambavyo vina sinonimu zenye asili ya Kiarabu, vilikusanywa na kuwekwa kwenye makundi kulingana na idadi ya maneno katika seti moja ya sinonimu. Kwa kutumia njia hii, jumla ya seti 71 za sinonimu zilikusanywa. Data zote zilizokusanywa zimetumika katika makala hii.

Data zilizokusanywa zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaudhui. Mbinu hii inahusisha uwekaji wa data katika makundi yanayofanana au kuhusiana. Kwa hiyo, seti za sinonimu zilizokusanywa zimewekwa katika makundi yanayofanana au kuwiana kiidadi. Mathalani, data zinazohusu seti za sinonimu ambazo zinahusisha maneno mawili ziliwekwa katika kundi lake. Vivyo hivyo, kwa data ambazo zinahusisha seti zenye maneno matatu au manne nazo ziliwekwa kwenye makundi yake kisha kufafanuliwa. Pamoja na mbinu hiyo, uchambuzi wa data pia umeongozwa na Nadharia ya Vijenzi Semantiki.

4.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Vijenzi Semantiki. Nadharia hii inaegemea katika msingi kuwa maneno yanajengwa na vijenzi fulani ambavyo hubainishwa kwa ajili ya kuelezea kila neno (Geeraerts, 2009; Kahigi, 2019). Vijenzi vya kila neno ndivyo vinavyounda maana ya jumla ya kila neno na ndivyo hutofautisha au kuonesha uhusiano uliopo baina ya maneno yaliyo katika kikoa kimoja. Kwa hiyo, ikiwa maneno mawili au zaidi yana vijenzi vinavyofanana au kukaribiana, maneno hayo yana sifa ya usinonimia. Nadharia hii hutumia alama ya jumlisha (+) kuashiria kuwapo kwa kijenzi maana husika na alama ya kutoa (-) kuashiria kutokuwapo kwa sifa au kijenzi husika katika neno. Vijenzi semantiki katika makala hii vinapatikana kutokana na fasili zinazotolewa na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 4* ambayo ndiyo msingi wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Kahigi (2019) anafafanua nadharia hii kwa kutumia data katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Kikoa cha Maana cha Samani

Kategoria ya Samani	**Vijenzi Maana**			
	Kiegemeo cha Nyuma	**Yenye Miguu**	**Sehemu ya Kukalia**	**Enye Vishikio**
Kiti	+	+	+	-
Sofa	+	+	+	+

Chanzo: Kahigi (2019)

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa kiti cha kawaida na sofa vinafanana katika vijenzi semantiki vitatu vya *kiegemeo cha nyuma, chenye miguu na kuwa* na *sehemu ya kukalia.* Hivyo, maneno hayo yana sifa ya kuwa sinonimu ingawa yanatofautiana katika dhana ya kuwa au kutokuwa na vishikizio kwa kuwa si mara zote kiti kinakuwa na vishikio kama ilivyo kwa sofa. Kwa hiyo, Nadharia ya Vijenzi Semantiki imetumika kubainisha maneno yenye maana zinazofanana au kukaribiana, yaani sinonimu kutoka katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 4* kwa kuangalia mfanano wa vijenzi semantiki vya maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu.

5.0 Ruwaza Zinazojitokeza kwenye Sinonimu za Mkopo kutoka Lugha ya Kiarabu

Data zilizokusanywa kutoka *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 4* (2019) zinaonesha kuwa lugha ya Kiswahili ina sinonimu za mkopo kutoka lugha ya Kiarabu. Kuwapo kwa sinonimu hizi kunatokana na lugha ya Kiswahili kukopa maneno mengi kutoka lugha ya Kiarabu. Jumla ya seti 71 za sinonimu zimekusanywa kutoka katika matini teule. Data zilizokusanywa zimewekwa katika makundi kulingana na idadi ya maneno katika seti moja ya sinonimu. Kulingana na uwekaji huo wa data, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza sita za sinonimu zinazohusisha maneno kutoka Kiarabu tu. Ruwaza zilizobainika ni pamoja na ruwaza ya uwili ambayo ina seti 20 sawa na 28%, ya utatu ambayo ina seti 18 sawa na 25%, ya unne ambayo ina seti 14 sawa na 20%, ya utano yenye seti 11 sawa na 15.5%, ya usita ambayo ina seti 6 sawa na 8.5, na ya usaba ambayo ina seti 2 za sinonimu sawa na 3%. Katika ubainishaji wa sinonimu hizo, vijenzi maana vya jumla vimebainishwa kwa kutumia alama ya kujumlisha (+) ili kuonesha uhusiano wa kimaana uliopo ambao ndio unaoibua sinonimu. Vijenzi maana vinavyotumiwa katika makala hii ni fasili za vidahizo zilizotolewa katika kamusi teule. Vijenzi maana vilivyotumika ni vile vya jumla ambavyo vinajitokeza katika memba wote hata kama kuna tofauti za urejeleo au matumizi katika memba husika. Ufafanuzi wa ruwaza zinazojitokeza kwenye sinonimu za mkopo kutoka Kiarabu unatolewa katika vipengele vinavyofuata.

5.1 Ruwaza ya Uwili wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Data za makala hii zinaonesha kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza za uwili wa sinonimu zinazohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Ruwaza ya uwili inahusisha maneno mawili katika seti ya sinonimu. Maneno hayo yote yamekopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Katika data zilizokusanywa, imebainika kuwa kuna seti 20 za sinonimu zinazohusisha ruwaza za uwili. Kwa ufafanuzi zaidi tutazame data katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Ruwaza ya Uwili wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Na.	Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu		Dhana Inayorejerewa
	Safu A	Safu B	
1.	kibatari	kibahaluli	+taa ndogo ya chupa au kopo yenye utambi inayotumia mafuta ya taa
2.	binti	banati	+mtoto wa kike wa mtu fulani
3.	bikira	batuli	+mwanamke ambaye kizinda chake hakijavunjwa
4.	karama	buruhani	+kipawa kutoka kwa Mungu
5.	starehe	burudani	+shughuli inayofanywa kwa ajili ya kufurahisha au kuchangamsha watu
6.	tabiri	bashiri	+eleza au toa habari ya mambo yatakayotokea kwa kutumia ujuzi au kwa kutafsiri ndoto au ishara

Na.	Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu		Dhana Inayorejerewa
	Safu A	**Safu B**	
7.	sehemu	akisami	+sehemu ya kitu; robo, nusu
8.	salimu	sabahi	+taka mtu hali
9.	barua	waraka	+maandishi yenye ujumbe yanayopelekwa kwa mtu mwingine kwa madhumuni ya kuarifu
10.	taratibu	halahala	+kwa taratibu
11.	bahatisha	kadiria	+jaribu kupata jambo bila ya kujua matokeo yake.
12.	bakora	henzirani	+fimbo ya kutembelea +pigo la fimbo
13.	baragumu	siwa	+pembe kubwa na ndefu iliyotobolewa tundu katika ncha yake inayopigwa katika ngoma au kutoa habari
14.	rafiki	sahibu	+mtu anayependwa sana na watu
15.	malaya	kahaba	+mtu anayefanya mambo ya uasherati
16.	herufi	hati	+maandishi ya mkono
17.	shetani	ibilisi	+shetani mkubwa miongoni mwa majini
18.	mnyororo	silisili	+vikuku vya chuma vilivyoshikamana kama mkufu
19.	sifuri	bila	+nambari 0 isiyokuwa na idadi ikiwa peke yake
20.	fitini	fisidi	+tia ugomvi baina ya mtu

Chanzo: KKS4 (2019)

Data katika Jedwali Na. 2 zinaonesha seti za sinonimu zinazohusisha maneno kutoka lugha moja ya Kiarabu. Maneno kama *kibatari/kibahaluli, binti/banati, bikira/batuli, karama/buruhani, starehe/burudani* ni sinonimu kwa sababu yanafanana katika vijenzi maana vyake. Pia, seti kama *tabiri/bashiri, sehemu/akisami, salimu/sabahi, barua/ waraka, taratibu/halahala, bahatisha/kadiria, bakora/henzirani, mnyororo/silisili,* na maneno mengine katika Jedwali Na. 2 nayo ni sinonimu kwa kuwa yanafanana katika vijenzi maana. Vijenzi maana hivyo vimeoneshwa katika safuwima ya dhana inayorejelewa, hivyo, ni sinonimu. Maneno kama *silisili* na *mnyororo* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanafanana katika dhana ya *vikuku vya chuma vilivyoshikamana kama mkufu*. Aidha, maneno *bakora* na *henzirani* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanafanana katika kijenzi semantiki ambacho ni *fimbo ya kutembelea*. Neno *rafiki* na *sahibu* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanafanana sana katika dhana ya *mtu anayependwa sana na watu*. Neno *sifuri* na *bila* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanafanana katika dhana ya *nambari 0 isiyokuwa na idadi ikiwa peke yake.* Hivyo, maneno hayo ni sinonimu zinazotoka lugha ya Kiarabu. Ruwaza hii iliwahi kubainishwa na watafiti tangulizi kama Ullmann (1967) katika lugha ya Kiingereza na Kifaransa na Kitundu (2022) katika lugha ya Kiswahili hususani kwenye sinonimu za asili na za mkopo.

5.2 Ruwaza ya Utatu wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya utatu ya sinonimu zinazohusisha maneno matatu ya Kiswahili yaliyokopwa kutoka lugha moja ya Kiarabu. Kuwapo kwa ruwaza hii kunatokana na lugha ya Kiswahili kukopa maneno mengi kutoka lugha ya Kiarabu kiasi kwamba kuna maneno matatu yanayorejelea dhana ileile au inayofanana, yaani sinonimu. Ruwaza hii ina jumla ya seti 18 za sinonimu zinazohusisha maneno ya Kiswahili yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ruwaza hii tutazame data katika Jedwali Na. 3.

Jedwali Na. 3: Ruwaza ya Utatu wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Na.	Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu			Dhana Inayorejerewa
	Safu A	Safu B	Safu C	
1.	juha	baghani	baghami	+mtu mwenye akili kidogo/ndogo
2.	adimika	ghaibu	ghalika	+patikana kwa uchache au kwa nadra
3.	daima	dahari	abadi	+siku zote
4.	afya	siha	rai	+hali nzuri ya mwili +bila ya maradhi
5.	ahadi	makubaliano	maafikiano	+tokeo la kukubaliana
6.	dawati	almari	jarari	+mtoto wa meza
7.	laumu	shutumu	aili	+toa mtu makosa
8.	kamilisha	akidi	timiza	+bila ya kuzidi wala kupungua
9.	arifu	taarifu	simulia	+julisha mtu habari ya jambo fulani
10.	faragha	nafasi	hatua	+mahali patupu
11.	jumuia	ushirika	kaumu	+kikundi cha watu
12.	ujeuri	ufidhuli	usafihi	+hali ya kuwa na tabia ya ufidhuli
13.	dhoruba	tufani	halibari	+mchafuko wa bahari +upepo mkali
14.	kasirika	hamaki	ghadhibika	+kuwa na hasira/shikwa na hasira
15.	adhabu	rada	ikabu	+balaa inayotoka kwa mwenyezi Mungu
16.	hubiri	simulia	hutubu	+toa nasaha za kidini
17.	taratibu	kaida	kawaida	+taratibu au kanuni ambazo hazina budi kufuatwa

Na.	**Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu**			**Dhana Inayorejerewa**
	Safu A	**Safu B**	**Safu C**	
18.	shetani	jini	habithi	+mtu mwovu au mwenye matendo mabaya

Chanzo: KKS4 (2019)

Data katika Jedwali Na. 3 zinaonesha seti za sinonimu zinazotokana na maneno ya Kiswahili ambayo yamekopwa kutoka Kiarabu. Seti hizo zinahusisha maneno matatu tofauti lakini yenye maana inayofanana au kukaribiana. Maana hiyo imebainishwa katika safuwima ya dhana inayorejelewa. Kwa mfano, maneno kama *juha/baghami/baghani* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *mtu mwenye akili kidogo.* Pia, maneno kama *adimika/ghaibu/ghalika* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *patikana kwa uchache au kwa nadra*. Halikadhalika, maneno *daima/dahari/abadi* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *siku zote*. Seti ya maneno *afya/siha/rai* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *hali nzuri ya mwili.* Maneno kama *ahadi/makubaliano/maafikiano* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana *tokeo la kukubaliana.* Vilevile, maneno kama *dawati/almari/jarari* ni sinonimu kwa sababu yanahusiana katika dhana ya *meza inayotumika kwa kazi mbalimbali kama vile kuandikia na/au kuwekea vitu*. Seti ya maneno *dhoruba/halibari/tufani* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanafanana katika dhana ya *mchafuko wa bahari/upepo mkali*. Aidha, maneno kama *shetani/jini/habithi* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *mtu mwovu au mwenye matendo mabaya*. Seti ya maneno kama *hubiri/simulia/hutubu* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *toa nasaha za kidini*. Seti zingine kama *arifu/taarifu/simulia, faragha/nafasi/hatua, kasirika/hamaki/ghadhibika, jumuia/ushirika/kaumu* ni sinonimu. Ruwaza hii ya utatu pia iliwahi kubainishwa na Ullmann (1967) katika lugha ya Kiingereza na Kifaransa pamoja na Kitundu (2022) katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, ruwaza zilizobainishwa na wataalamu hao zilihusisha neno la asili na la mkopo katika lugha walizotafiti wakati makala hii imechunguza maneno ya mkopo tu kutoka lugha moja ya Kiarabu.

5.3 Ruwaza ya Unne ya Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya unne wa sinonimu ambayo inahusisha maneno manne katika seti moja ya sinonimu. Maneno hayo yanatoka katika lugha moja tu ya Kiarabu. Hii ina maana kuwa kutokana na kuwapo kwa mwingiliano wa jamiilugha ya Kiswahili na Kiarabu, wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili wamekopa maneno manne kutoka Kiarabu ambayo yanarejelea dhana moja au ileile, hivyo, kuibua seti ya sinonimu yenye maneno manne. Kulingana na data

zilizokusanywa, imebainika kuwa kuna seti 14 za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya unne. Kwa ufafanuzi zaidi tutazame data katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Ruwaza ya Unne wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Na.	Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu				Dhana Inayorejerewa
	Safu A	**Safu B**	**Safu C**	**Safu D**	
1.	katu	abadani	asilani	halisi	+hata kidogo
2.	binadamu	adinasi	mahuluku	insi	+kiumbe aghalabu hutembea wima mwenye kuumbwa
3.	heshimu	jali	stahi	thamini	+weka adabu +fanyia heshima
4.	sawasawa	naam	sadakta	halisi	+kama inavyotakiwa
5.	sadaka	dhabihu	kafara	edaha	+kitu chochote kinachotolewa kwa Mungu au mizimu kwa ajili ya jambo fulani
6.	kusudia	nuia	azimu	hirimia	+taka kwa nia
7.	ashiki	mashamshamu	hanjamu	hawaa	+hali ya kuwa katika hekaheka
8.	laghai	ayari	kahini	bazazi	+mtu mdanganyifu
9.	mahabubu	muhibu	hababi	shabiki	+mpenzi wa kike au kiume
10.	shujaa	jabari	abtari	ghazi	+mtu mwenye moyo thabiti mwenye uwezo wa kukabili mambo hata kama ni ya hatari
11.	aminika	kubalika	sadikika	tasawari	+wezekana kukubaliwa
12.	maskini	fukara	fakiri	dhahili	+mtu asiyekuwa na pato la kutosha
13.	fikiri	tafakari	taamali	kadiri	+kuwa na wazo +fikiria jambo kwa makini
14.	samehe	bihi	feleti	dhamini	+acha mtu huru baada ya kutenda kosa fulani

Chanzo: KKS4 (2019)

Jedwali Na. 4 linaonesha seti za sinonimu za mkopo kutoka lugha ya Kiarabu. Katika data hiyo, kila seti ya sinonimu inahusisha maneno manne ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Maneno hayo ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana inayorejelewa kwenye safuwima ya dhana inayorejelewa. Mathalani, seti ya sinonimu *laghai/ayari/kahini/bazazi* ni sinonimu kwa kuwa zinahusiana katika dhana ya *mtu mdanganyifu*. Halikadhalika, seti ya sinonimu *mahababu/muhibu/hababi/shabiki* nayo ni sinonimu kwa kuwa maneno hayo yanahusiana katika dhana ya *mpenzi wa kike au kiume.* Maneno

katu/abadani/asilani/halisi, nayo yana sifa ya usinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *hata kidogo.* Aidha, seti ya maneno *heshima/jali/stahi/thamini,* nayo yana sifa ya usinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *weka adabu/fanyia heshima.* Maneno kama *sadaka/dhabihu/kafara/eda/edaha* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *kitu chochote kinachotolewa kwa Mungu au mizimu kwa ajili ya jambo fulani.* Seti ya maneno *maskini/fukara/fakiri/dhahili* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *mtu asiyekuwa na pato la kutosha*.

Aidha, seti ya maneno *sawasawa*/*eda/dhabihu/kafara* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *kama inavyotakiwa.* Pia, seti ya maneno *kusudia/nuia/hirimia/azimu* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *taka kwa nia.* Aidha, maneno *mashamshamu/hanjamu/hawaa* na seti *shujaa/jabari/abtari/ghazi* nazo ni sinonimu kwa kuwa zinafanana katika vijenzi semantiki. Ruwaza hii ya unne iliwahi kubainishwa na Kitundu (2022) katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kwa tafiti tangulizi zilizochunguza ruwaza ya sinonimu katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kialbani hazikubainisha ruwaza hii.

5.4 Ruwaza ya Utano wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya sinonimu inayohusisha maneno matano ya Kiswahili yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Kulingana na data zilizokusanywa, imebainika kuwa kuna seti 11 za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya utano. Kuwapo kwa ruwaza hii kunamaanisha kuwa lugha ya Kiswahili imekopa maneno matano yenye maana sawa au zinazokaribiana kutoka lugha ya Kiarabu. Data za ruwaza hii ya utano zinawasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Ruwaza ya Utano wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Na.	Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu					Dhana Inayorejerewa
	Safu A	Safu B	Safu C	Safu D	Safu E	
1.	baa	balaa	nuksi	beluwa	balia	+jambo au tukio linaloleta maafa, hasara au shida
2.	dhani	fikiri	shuku	tuhumu	hesabu	+kutokuwa na uhakika kamili
3.	kubali	afiki	ridhia	hiari	ridhika	+toa ruhusa ya kitu kifanyike pokea wazo, wito au tendo
4.	dosari	walakini	taksiri	taathira	mushkili	+hali inayopunguza ukamilifu wa kitu

5.	msaada	auni	nusura	muawana	amara	+hali au kitu anachotoa mtu, nchi ili kutimiza haja ya mtu au nchi nyingine
6.	laghai	hadaa	kadhibu	ghuri	ghilibu	+fanyia hila +sema uongo
7.	zawadi	tuzo	hidaya	hadia	azizi	+kitu kinachotolewa bure bila malipo
8.	haraka	arubii	halani	ajilani	dalihini	+upesi/mara moja
9.	amri	sharti	lazima	dikrii	faradhi	+jambo au kitu cha lazima
10.	juhudi	kasi	idili	hima	ari	+hali ya kutaka kukamilisha jambo +kutotaka kushindwa
11.	dhaifu	nyonge	dhalili	dhuli	tuli	+hali ya chini +enye kudharauliwa

Chanzo: KKS4 (2019)

Jedwali Na. 5 linaonesha seti 11 za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya utano. Katika Jedwali hilo, seti ya maneno *baa/balaa/nuksi/beluwa/balia* ni sinonimu zinazohusiana katika dhana ya *jambo au tukio linaloleta maafa, hasara au shida.* Vilevile, seti ya maneno *dhani/fikiri/shuku/tuhumu/hesabu* ni sinonimu kwa kuwa zinahusiana katika dhana ya *kutokuwa na uhakika kamili.* Pia, seti ya maneno kama *msaada/auni/nusura/muawana/amara* nayo ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *hali au kitu anachotoa mtu, nchi ili kutimiza haja ya mtu au nchi nyingine*. Seti ya maneno *kubali/afiki/ridhia/hiari/ridhika* ni sinonimu kwa kuwa zinahusiana katika dhana ya *toa ruhusa ya kitu kifanyike.* Aidha, seti ya maneno *dhaifu/nyonge/dhalili/dhuli/tuli* ni sinonimu kwa kuwa zinagusiana katika kijenzi maana cha *hali ya chini.* Ruwaza hii iliwahi kubainishwa pia na Kitundu (2022) katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, Kitundu alichunguza sinonimu za asili na za mkopo ilhali utafiti huu umechunguza sinonimu za mkopo tu kutoka Kiarabu.

5.5 Ruwaza ya Usita ya Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya usita ya sinonimu za mkopo kutoka Kiarabu. Ruwaza hii inahusisha maneno sita ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Kuwapo kwa ruwaza hii kunatokana na kuwapo kwa ukopaji wa maneno kutoka lugha ya Kiarabu jambo ambalo limesababisha kuwe na maneno sita yenye kuhusiana

kimaana, yaani sinonimu. Kulingana na data zilizokusanywa imebainika kuwa kuna seti 6 za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya usita. Data zinazohusisha ruwaza hii zimewasilishwa katika Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 6: Ruwaza ya Usita wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Na.	Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu						Dhana Inayorejerewa
	Safu A	Safu B	Safu C	Safu D	Safu E	Safu F	
1.	bora	azizi	aula	afadhali	heri	falau	+enye thamani +tunu
2.	hirizi	dawa	talasimu	azima	amali	majuni	+kitu kinachovaliwa mwilini au mkononi kinachoaminiwa kuwa ni dawa ya kujikinga na madhara
3.	dhihaka	kebehi	kejeli	stihizai	utani	masihara	+maneno au vitendo vya kuudhi vifanyavyo kwa masihara
4.	ridhaa	idhini	ikibali	hiari	kibali	ruhusa	+uchaguzi wa kutenda jambo bila kulazimishwa
5.	dhiki	shida	taabu	udhia	adha	madhila	+jambo linalosumbua au kuleta shida
6.	nafuu	ahueni	afadhali	shufaa	hujambo	tahafifi	+nafuu apatayo mtu baada ya matatizo au ugonjwa

Chanzo: KKS4 (2019)

Jedwali Na. 6 linaonesha seti za sinonimu zinazohusisha maneno 6 ya Kiswahili ambayo yamekopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Maneno hayo ni sinonimu kwa sababu yanahusiana katika dhana inayofanana ambayo imeoneshwa katika safuwima ya dhana inayorejelewa. Mathalani, seti ya maneno *bora/azizi/aula/afadhali/heri/falau* yanahusiana katika dhana ya *enye thamani/tunu/vyema zaidi*. Hivyo, maneno hayo ni sinonimu. Pia, seti ya maneno *dhihaka/kebehi/kejeli/stihizai/utani/masihara* inahusiana katika dhana ya *maneno au vitendo vya kuudhi vifanyavyo kwa masihara.* Hivyo, seti hiyo ina sifa ya kuwa sinonimu. Vilevile, seti ya maneno *dhiki/shida/taabu/udhia/adha/madhila* inahusiana katika dhana ya *jambo linalosumbua au kuleta shida*. Hivyo, seti hiyo ni sinonimu. Seti ya maneno *hirizi/dawa/talasimu/azima/amali/majuni* ni sinonimu kwa kuwa maneno yake yanahusiana katika kijenzi semantiki *kitu kinachovaliwa mwilini au mkononi kinachoaminiwa kuwa ni dawa ya kujikinga na madhara.*

Seti ya maneno *nafuu/ahueni/afadhali/shufaa/hujambo/tahafifi* nayo ina sifa ya kuwa sinonimu kwa kuwa maneno yake yanafanana katika kijenzi maana cha *nafuu apatayo mtu baada ya matatizo ya ugonjwa*. Pia, seti ya maneno

dhiki/*shida/taabu/udhia/adha*/*madhila* nayo ni sinonimu kwa kuwa inahusiana katika kijenzi maana cha *jambo linalosumbua au kuleta shida*. Vilevile, seti yenye maneno *hirizi/dawa/talasimu/azima/amali/majuni* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika kijenzi maana cha *kitu kinachovaliwa mwilini au mkononi kinachoaminiwa kuwa ni dawa ya kujikinga na madhara.* Aidha, seti ya mneno *ridhaa/idhini/ikibali/hiari/kibali/ruhusa* yana sifa ya usinonimu kwa kuwa yanafanana katika kijenzi maana *uchaguzi wa kutenda jambo bila kulazimishwa.* Ruwaza hii ya usita haikuwahi kubainishwa na tafiti tangulizi kama Ullamnn (1967), Resani (2015), Chacha na Malangwa (2019) na Kitundu (2022). Hivyo, ni jambo jipya ambalo limeibuka katika makala hii.

5.6 Ruwaza ya Usaba wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Lugha ya Kiswahili ina ruwaza ya usaba wa sinonimu. Ruwaza ya usaba inahusisha maneno 7 ya Kiswahili ambayo yamekopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Ruwaza hii ina jumla ya seti mbili za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya usaba. Ruwaza hii unapoilinganisha na ruwaza nyingine inajitokeza kwa uchache. Hivyo, ni dhahiri kuwa kuna ujitokezaji mdogo wa ruwaza ya usaba kuliko ruwaza zingine. Data za ruwaza hii zinawasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 7.

Jedwali Na. 7: Ruwaza ya Usaba wa Sinonimu za Mkopo kutoka Kiarabu

Na.	Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu							Dhana Inayorejerewa
	Safu A	Safu B	Safu C	Safu D	Safu E	Safu F	Safu G	
1.	tukufu	adhimu	jalili	aali	ashirafu	ali	akrama	+enye sifa iliyotukuka
2.	kashfa	aibu	junaa	izara	hizaya	fedheha	haya	+udhihirisho wa siri ya jambo la aibu +jambo limvunjialo mtu aibu

Chanzo: KKS4 (2019)

Jedwali Na. 7 linaonesha seti mbili za sinonimu zinazohusisha ruwaza ya usaba. Katika seti hizo, maneno *aali/adhimu/jalili/tukufu/ashirafu/ali/akrama* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *-enye sifa iliyotukuka*. Pia, seti ya maneno *kashfa/junaa/izara/hizaya/fedhaha/aibu/haya* ni sinonimu kwa kuwa yanahusiana katika dhana ya *udhihirisho wa siri ya jambo la aibu/jambo limvunjialo mtu aibu*. Ruwaza hii haikuwahi kubainika katika tafiti mbalimbali alizopitia mtafiti kama vile Ullmann (1967), Chacha na Malangwa (2019) na Kitundu (2022). Hivyo ni jambo jipya.

Kwa ujumla, kulingana na uchambuzi na uchanganuzi wa data imebainika kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza za sinonimu zinazohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Kuwapo kwa ruwaza hizi kunatokana na Kiswahili kukopa maneno mengi kutoka Kiarabu kutokana na kuwapo na

muwasala wa muda mrefu. Kiango (1999) aliwahi kusema kuwa wazungumzaji wa lugha (ya Kiswahili) wana tabia ya kukopa msamiati kutoka lugha ngeni hata kama msamiati wanaokopa walikwisha kuukopa hapo awali. Hali hii inajidhihirisha katika makala hii ambapo tunaona kuwa kuna maneno mengi ya Kiswahili yaliyokopwa kutoka lugha moja ambayo yanarejelea dhana ileile. Mathalani, kuna maneno saba ambayo yanarejelea dhana moja kutoka lugha ya Kiarabu. Hii inamaanisha kuwa wazungumzaji wa Kiswahili walikopa maneno saba yenye kufanana kimaana kutoka lugha ya Kiarabu. Ruwaza zilizobainika katika makala hii ni sita. Ruwaza hizo ni uwili ambayo inahusisha maneno mawili, ruwaza ya utatu inayohusisha maneno matatu na ruwaza ya unne inayohusisha maneno manne. Ruwaza zingine zilizobainika ni ruwaza ya utano yenye maneno matano, ruwaza ya usita yenye maneno sita na ruwaza ya usaba ambayo inahusisha maneno saba. Kati ya ruwaza hizo, ruwaza ya uwili ina seti nyingi za sinonimu ukilinganisha na ruwaza nyingine. Ruwaza ya usaba ndio yenye seti chache zaidi kuliko ruwaza nyingine. Hii inatokana na ugumu uliopo wa kuwa na maneno mengi yanayorejelea dhana ileile kutoka lugha moja tu.

Ruwaza hizi ni zaidi ya zile zilizobainishwa na Ullmann (1967) katika lugha ya Kiingereza na Kifaransa ambao walibainisha ruwaza mbili, na ni zaidi ya zile zilizobainishwa na Kitundu (2022) katika lugha ya Kiswahili ambaye alibainisha ruwaza nne. Ingawa wataalamu hao walishughulikia sinonimu za asili na za mkopo lakini suala la ruwaza zilizojitokeza katika lugha walizotafiti linatofautiana na ruwaza hizi kwa kuwa kuna ongezeko la ruwaza mbili kutoka zile tano zilizobainishwa na Kitundu na kuna ongezeko la ruwaza nne kutoka zile mbili zilizobainishwa na Ullmann (1967).

6.0 Hitimisho

Makala hii inahitimisha kuwa lugha ya Kiswahili ina ruwaza sita za sinonimu zinazohusisha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Ruwaza hizo ni ruwaza ya uwili, ya utatu, ya unne, ya utano, ya usita na ya usaba. Kuwapo kwa ruwaza hizi kunatokana na lugha ya Kiswahili kukopa maneno mengi kutoka lugha ya Kiarabu. Ukopaji huu unatokana na kuwapo kwa mtagusano baina ya jamiilugha ya Waswahili na Waarabu. Kutokana na mtagusano huo, wazungumzaji wamekopa maneno mawili au zaidi kutoka lugha hiyo ambayo yana sifa ya sinonimu. Hali hii imeibua ruwaza mbalimbali za sinonimu za Kiswahili zenye asili ya Kiarabu. Kulingana na kuwapo kwa mtagusano wa jamiilugha hizi mbili kibiashara, kielimu, kimichezo na hata kisiasa upo wezekano wa ruwaza hizi kuongezeka kwa kuwa watumiaji wa lugha wana tabia ya kukopa maneno kila wanapotagusana na jamiilugha nyingine. Hivyo, kadiri ukopaji wa maneno unavyoendelea ndivyo na mabadiliko ya ruwaza yanavyotokea.

Marejeleo

Ahmad, S. (2021). Ulinganishi wa Maana za Maneno ya Kiswahili na Kiurdu yenye Asili ya Kiarabu. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bosha, I. (1994). Athari za Kiarabu katika Kiswahili Sanifu. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chacha, L.M. na Malangwa, P.S. (2019). *Semantiki.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Dar es Salaam University Press.

Chuwa, A.R. (1988). "Foreign Loan Words in Kiswahili". *Kiswahili,* Juz. 55(1) na (2): 163-172.

Cruse, A. (2006). *A Glossary of Semantics and Pragmatics.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Danglli, L. (2010). "Origin of Synonyms and their Acquisition as Vocabulary". *LCPJ Publishing,* Juz. 3(2): 66-72. Inapatikana katika https://www.lcpj.pro/skedaret/1355270481-Revista%20LCPJ_3_2_31.pdf. Ilisomwa Tarehe 25 Januari 2025.

Geeraerts, D. (2009). *Theories of Lexical Semantics.* New York: Oxford University Press.

Gibbe, A.G. (2010). *Homonymy, Synonymy and Antonym in Kiswahili: A Lexical Study*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Grey, L.H. (1964) *Foundations of Language.* New York: The Macmillan Company.

Habwe, J., Matei, A., na Nyonje, J. (2010). *Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyuo.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hoffer, B.L. (2005). "Language Borrowing and the Indices of Adaptability and Receptivity". *Intercultural Communication Studies,* Juz. 14(2): 53-72. Inapatikana katika https://web.uri.edu/iaics/files/05-Bates-L.-Hoffer.pdf. Ilisomwa tarehe 20 Januari 2025.

Kahigi, K.K. (2019). *Misingi ya Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Kiango, J.G. (1999). "Matatizo ya Utohozi wa Maneno kama Mbinu ya Kukopa Istilahi katika Lugha". *Mulika,* Juz. 25: 1-8.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii.* Dar es Salaam: TUKI.

Kitundu, G.J. (2022). Ruwaza Zinazojitokeza kwenye Sinonimu za Asili na za Mkopo katika Kiswahili. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Krumm, B. (1940). *Words of Oriental Vrigin in Swahil*. London: Sheldon Press.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, M. (2010). A Study of Adaptation of Arabic Loanwords in Kiswahili: A Case of *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004).* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mzamir, I. (2021). Uchambuzi wa Kietmolojia na Uainishaji wa Maneno yenye Asili ya Kiarabu katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili Toleo la 2 (2017).* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ndimele, O. (1997). *Semantics and the Frontiers of Communication*. Port Harcourt: University of Port Harcourt Press Ltd.

Nurse, D. na Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the History and Language of an African Society.* Philadelphia: University of Pennsylvania.

Resani, M. (2015). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Print Technology.

Robins, R.H. (1980). *General Linguistics.* London: Longmans.

Shembilu, M.M. (2017). Michakato ya Kisemantiki kwenye Maneno ya Mkopo katika Kiswahili: Mifano kutoka Kiingereza na Kiarabu. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 4*. Nairobi: Oxford University Press.

Ullmann, S. (1967) *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. London: Oxford.

Wittgenstein, L. (1953). *Philosophical Investgations*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.